**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA**

**SHULE YA SEKONDARI NYAMPULUKANO**
**S.L.P 104**
**SENGEREMA**

**Kumb. Na.NY/SS/JI/F5/09** **29/3/2022**

**MKUU WA SHULE; 0763199736**

**MAKAMU MKUU WA SHULE ;0764727499/0757302314**

**Jina la mwanafunzi....................................................................**

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAMPULUKANO ILIYOPO WILAYA YA SENGEREMA MKOA WA MWANZA KWA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023

**1.0. UTANGULIZI**.

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **kidato cha tano (5)** katika shule hii **mwaka 2022/2023.** Shule ya sekondari ya Nyampulukano ipo umbali wa km 2 $\frac{1}{2}$ Kaskazini Magharibi kutoka mji mkuu wa Halmashauri ya wilaya ya **Sengerema** . Nauli kutoka mjini ni Tsh 4000 kwa taksi na Tsh.1000 kwa pikipiki/bajaji. Masomo yataanza **tarehe ……………… hivyo** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **tarehe …………….. na** mwisho wa kuripoti ni **tarehe …………………** kabla ya saa 11:00 jioni. Wanafunzi ambao hawataripoti ndani ya wiki mbili tangu tarehe ya kufungua shule nafasi zao zitachukuliwa na wanafunzi wengine ambao hawakupangiwa shule katika awamu hii.

## 2.0; MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1. ADA NA MICHANGO YA SHULE

- **Ada ya shule** ni Tsh **70,000/=** kwa mwaka. Ilipwe kwa mkupuo Tsh **70,000/=** au Tsh **35,000/=** mwanzoni mwa kila muhula. Fedha za ada zilipwe kwenye;-

  **-**Akaunti **Na. 31601200072** NMB tawi lolote Tanzania.

  **-**Jina la akaunti;-**Nyampulukano Secondary School Recurrent Account.**

- **Michango ya shule. Tsh. 118,000/= kwa mwaka**

  Fedha za michango ya shule zilipwe kwenye;-

  **-** Akaunti **Na. 31602300144 NMB** tawi lolote Tanzania.

  **-**Jina la akaunti ni:-**Elimu ya Kujitegemea Nyampulukano Sekondari.**

  **Stakabadhi ya benki iandikwe jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi yake kwa juu na nyuma mgawanyo wa malipo yaliyofanyika.**

- **MCHANGANUO WA FEDHA KWA AJILI YA ADA NA MICHANGO MBALIMBALI**

| **MCHANGO WA** | **KIASI** | **AKAUNTI** |
|---|---|---|
| **ADA** | **70,000/=** | Name; **NYAMPULUKANO S. S.**<br>No; **31601200072 -NMB** |
| Tahadhari (hazitarudishwa) | 5,000/= | Name; **E.K. NYAMPULUKANO SEKONDARI**<br>No; **31602300144 -NMB** |
| Uendeshaji wa mitihani ya kujipima | 20,000/= | |
| Bima CHIF | 6,000/= | |
| Nembo | 2,000/= | |
| Kitambulisho | 6,000/= | |
| Ukarabati | 15,000/= | |
| Wapishi & walinzi | 30,000/= | |
| Gharama ya maji na umeme | 15,000/= | |
| Taaluma | 15,000/= | |
| Huduma ya kwanza (michezo) | 4,000/= | |
| Jumla | 118,000/= | |
| **JUMLA YA ADA NA MICHANGO** | **188,000/=** | |

- ## SARE YA SHULE

1. **Kwa mwanafunzi wa kike.**
   - (a) Sketi mbili (2) ndefu usawa wa enka za rangi ya kijani-bluu(aquagreen) namba 1 zenye rinda box mbele na nyuma na marinda matatu kila upande kwa matumizi ya darasani.
   - (b) Sketi mbili ndefu usawa wa enka za rangi ya kaki namba 1 zenye rinda box mbele na nyuma na marinda matatu kila upande kwa matumizi baada ya vipindi.
   - (c) Shati mbili zenye mikono mirefu za rangi nyeupe zisizo na urembo za kufungwa kwa vishikizo vya kawaida.
   - (d) Fulana 2 za rangi ya dark-blue zenye ukosi wa kaki wenye mistari ya darkblue zisizo na maandishi (kwa matumizi baada ya vipindi vya darasani).
   - (e) Fulana 1 rangi ya kijani jeshi zisizo na ukosi na zisizo na maandishi kwa matumizi ya michezo. Kwa wasichana wa kiislam watavaa half kanzu yenye rangi ya T-shirt.
   - (f) Viatu vyeusi jozi mbili(2) vya ngozi vyenye kutumia rangi na vinavyofungwa na kamba.
   - (g) Soksi nyeupe zisizo na marembo jozi mbili
   - (h) Sweta 1 rangi ya kijani kisamvu
   - (i) Tai mbili (2) za rangi ya sketi (bluu kijani – aqua green).
   - (j) Track suit nyeusi zenye michirizi myeupe kwa ajili ya michezo.
   - (k) Raba nyeupe pair 1 kwa ajili ya michezo na baada ya vipindi vya darasani.

     **NB:** **Wanafunzi wa kiislamu watatumia hijabu ndefu inayofunika mabega nyeupe wakati wa vipindi na hijabu ndefu inayofunika mabega ya rangi ya pinki na blue bahari baada ya vipindi.**
2. **Kwa wanafunzi wa kiume**.
   - (a) Suruali mbili (2) zenye marinda 2 kila upande na mifuko 3 za rangi ya kijani-bluu (aqua – green) namba 1 zisizobana mwili kwa ajili ya darasani

(b) Suruali 2 zenye marinda 2 kila upande na mifuko 3 za rangi ya kaki namba 1 zisizobana mwili kwa matumizi matumizi baada ya vipindi.
(c) Shati mbili (2) zenye (2) zenye mikono mirefu za rangi nyeupe zisizo na urembo za kufungwa kwa vishikizo vya kawaida.
(d) Fulana 2 za rangi ya dark-blue zenye ukosi wa kaki wenye mistari ya darkblue zisizo na maandishi (kwa matumizi baada ya vipindi vya darasani).
(e) Fulana 1 rangi ya kijani zisizo na ukosi na zisizo na maandishi kwa matumizi ya michezo.
(f) Viatu vyeusi jozi mbili(2) vya ngozi vyenye kutumia rangi na vinavyofungwa na kamba.
(g) Soksi nyeusi zisizo na marembo jozi mbili
(h) Sweta 1 rangi ya kijani
(i) Tai mbili (2) za rangi ya sketi (bluu kijani – aqua green).
(j) Track suit nyeusi zenye michirizi myeupe kwa ajili ya michezo.
(k) Raba nyeupe pair 1 kwa ajili ya michezo na baada ya vipindi vya darasani na michezo.

NB:-**Kwa wale watakaopenda kushonewa/kuandaliwasare za shule katika mazingira ya shule, zinaweza kupatikana kwa gharama zifuatazo;-**

| | |
|---|---|
| Suruali 2 za darasani kwa wavulana @ 18,000/= | 36,000/= |
| Suruali 2 kwa kazi za nje ya darasa kwa wavulana @ 18,000/= | 36,000/= |
| Sketi 2 ndefu usawa wa enka za darasani kwa wasichana @ 23,000/= | 46,000/= |
| Sketi 2 ndefu usawa wa enka kwa kazi za nje ya darasa @ 23,000/= | 46,000/= |
| *Flana* 2 za dark-blue zenye ukosi wa kaki na nembo ya shule@ 10,000/= | 20,000/= |
| Tai 2 zenye nembo ya shule @ 3,000/= | 6,000/= |
| *Flana* ya michezo yenye nembo ya shule 1 @ 6,000/= | 6,000/= |
| Sweta lenye nembo ya shule 1 @ 12,000 | 12,000/= |
| **JUMLA. TSH.116,000/= kwa wavulana na TSH.136,000/= Kwa wasichana** | |

- **Ataruhusiwa kuja na sare ya shule atokayo au track – suit wakati akisubiria kupewa sare za shule yetu.**

- **Shule haipokei fedha taslimu**. Fedha zote zilipwe kwa kupitia Benki ya NMB, tawi lolote, kwa kutumia namba za akaunti husika na stakabadhi za malipo (Bank pay-in-slips) zenye jina la mwanafunzi ziletwe shuleni siku ya kuripoti. Mwanafunzi hatapokewa shuleni endapo hatakamilisha jumla ya fedha zote kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu

**MALAZI**

- **Godoro kwa wasichana ni 3.5x4x6 na kwa wavulana ni 2.5x4x6. Ili kuepuka usumbufu, Godoro linakodishwa shuleni kwa Tsh. 25,000/= kwa miaka miwili**
- Blanketi la kujifunika
- Chandarua rangi ya bahari(*light blue*) kwa wavulana na pinki kwa wasichana
- Mashuka 2 rangi ya bluu bahari kwa wavulana na pinki kwa wasichana.
- Mto na foronya (foronya rangi ya shuka).

**3. MAHITAJI MENGINE**

- **Taa ya *kuchaji kwa jua(solar)*** ama Taa ya betri kwa tahadhali ya umeme ukikatika (ISIWE YAKUCHAJI KWA UMEME)
- Bukta 1 rangi ya bluu
- Taulo
- Kanga kwa wasichana (jozi moja)
- Kandambili jozi moja
- Mafuta ya kupaka, Mswaki na dawa ya meno.
- Ndoo 1 (Lita 20), na dumu 1 dogo(Lita 5) kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
- Kijiko, sahani ya shaba, bakuli la shaba na kikombe kwa ajili ya uji.

**4 VIFAA VYA USAFI WA SHULE**

4.1 Mfagio wa ndani wenye mpini *(Soft broom)* 1
4.2 Jembe na mpini wake.
4.3 Chelewa ndefu ya nje (fagio la wima) 1. Iliyofungwa kwa wire.
4.4 Kotama (sickle) (wavulana) na ndoo ya lita 20 (wasichana).
4.5 Kwanja 1

**5 MAELEKEZO MENGINE**

5.1 Tarehe ya kufungua shule imeoneshwa hapo juu, ukichelewa kuripoti shuleni ndani ya siku kumi na nne utapoteza nafasi yako.
5.2 Uje na nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5.3 Uje na nakala ya hati yako ya matokeo ya kidato cha NNE (CSEE *results slip*).
5.4 Uje na barua hii na viambata vyake vyote vikiwa vimejazwa vema. Fomu ya uchunguzi wa afya ijazwe na daktari wa hospitali ya wilaya au teule.
**5.5 Nguo za nyumbani haziruhusiwi, mwanafunzi atavaa sare za shule muda wote awapo shuleni na asafiripo kuja shuleni au aendapo nyumbani.**
5.6 Kila mzazi /mlezi anapaswa kugharamia usafiri wa mwanae kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo na kumpa fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi. Ruhusa ya kufuata fedha za matumizi haitolewi. Mzazi unakumbushwa kuwa kumpa mwanao fedha inayopita kiasi, kwaweza kuchangia kuporomoka kwa taaluma yake.
**5.7** Asiyetimiza maelekezo tajwa hapo juu hatapokewa.
5.8 **Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu akiwa shuleni. (HARUHUSIWI KUMILIKI SIMU SHULENI)**

**NB;- Gharama za matibabu hospitali ya rufaa ama haspitali binafsi kila mwanafunzi atajigharamia. Hivyo kama mwanao kama ana bima ya afya aje nayo.**

**6.0. VIFAA VYA MASOMO**

- **Mabunda mawili (2) ya karatasi A4.*(Ream 2 Double A) kwa mwaka.***
- **Madaftari makubwa (Counter books) angalau kumi (10) au zaidi**
- **Kikokotozi (SCIENTIFIC CALCULATOR) kwa wanafunzi wa sayansi*(kwa kuepuka kuuziwa scientific calculator feki mwanafunzi/mzazi unashauriwa kuleta kiasi cha Tshs. 45,000/= shuleni ili kupewa calculator original ambayo haitamsumbua katika kujifunza)***

- **Mkebe wa zana za upimaji na sahani yake(Disecting kit)& tray kwa wanafunzi wanaosoma somo la Elimu ya viumbe(Biology)**
- **Kalamu za wino na za mkaa.**
- **mkebe wa hisabati**
- **Kila mwanafunzi aje na vitabu vya masomo yake. (Orodha ya vitabu imeambatishwa).**

## 7.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu ,Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa maelekezo zaidi mara baada ya kuripoti shuleni.

**NI LAZIMA KUFANYA MAMBO YAFUATAYO.**

(a) Heshima kwa viongozi ,wazazi , wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila kazi ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
(c) Kushiriki kufanya maandalio ya jioni [ Preparation], shuleni na usiku.
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(h) Kutunza mali ya umma
(i) Kutii wito, kuheshimu ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.
(j) Kuwa na nywele fupi wakati wote mwanafunzi awapo shuleni ( kwa jinsia zote)Nywele zisizidi urefu wa 0.5cm na ndevu zinyolewe wakati wote.
(k) Huruhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu bila idhini.

### 7.1. Makosa yanayoweza kusababisha kusimamishwa masomo /kufukuzwa shule;-

**i)** Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kuberi ,**sigara ,ugoro** n.k
**ii)** Wizi wa aina yoyote.
**iii)** Ubakaji, Uasherati na ushoga.
**iv)** Kupiga ama kupigana.(mwanafunzi vs mwanafunzi , mwanafunzi vs mtumishi,nk.)
**v)** Kudharau bendera ya taifa.
**vi)** Kuoa ama kuolewa.
**vii)** Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
**viii)** Kutoa mimba.
**ix)** Kugoma,kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule.
**x)** Kukataa adhabu kwa makusudi.
**xi)** Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
**xii)** Kuonekana kwenye nyumba za sitarehe na kumbi mbalimbali mfano: Nyumba za kulala wageni na baa.
**xiii)** Kuwa na pasi ya umeme, jiko la umeme na vifaa vingine vinavyoweza kusababisha ajali ya moto.

**xiv)** Kufanya jaribio lolote la kuua au kujiua au kutishia kujiua kwa kunywa sumu,kujichoma kisu, n.k
**xv)** Kutohudhuria masomo Zaidi ya siku 90 bila taarifa.
**xvi)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi, viongozi na jamii kwa ujumla.
**xvii)** Kusuka nywele, kufuga ndevu ama sharubu.
**xviii)** Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.

**ONYO**

Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo:-

(i) Kubana sare ya shule

**(ii)** Kuja shule na nguo za nyumbani**( Ataruhusiwa kuja na sare ya shule atokayo pamoja na track – suit 1 wakati akisubiria kupewa sare za shule yetu.)**

(iii) Kunyoa mitindo ( Panki, kiduku n.k)

(iv) Ni mwiko kumiliki vifaa vya umeme kama vile pasi.

(v) Ni mwiko kumiliki simu, vidani, vipodozi na perfume.

(vi) Ni mwiko kuja na vyakula shuleni na kupeleka vyakula bwenini.

(vii) Ni mwiko kutoka nje ya shule bila kibali. Endapo umeruhusiwa, tembea na kibali chako na urudi shuleni kwa wakati ulioelekezwa.

**(viii) MUDA WA KUINGIA SHULE MWISHO NI SAA 11:00 JIONI.**

8.0. **Mambo mengine muhimu**;

8.1. Fomu ya uambatisho wa afya(Medical examination form), ijazwe na Mganga wa Hospitali ya wilaya au Hospitali teule.

8.2. Fomu ya taarifa muhimu,ijazwe kikamilifu na kusainiwa na mzazi na mwanafunzi. Weka picha na namba sahihi za simu za wazazi/ walezi.

8.3. Fomu ya mkataba wa kutokushiriki migomo, fujo na makosa ya jinai,ijazwe na kusainiwa na mzazi na mwanafunzi.

8.4. Ulete kivuli cha cheti cha kuzaliwa na result slip ya CSEE

**NB.** Tafadhali fomu hizi ziletwe siku ya kuripoti shuleni.

***Moto wa Shule*: ELIMU KWA MAENDELEO;**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

MKUU WA SHULE
...MPULUKANO SHULE YA SEKONDARI
S.L.P. 104
SENGEREMA

**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA**
**SHULE YA SEKONDARI YA NYAMPULUKANO**

**FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

1 .Jina kamili la mzazi/mlezi-------------------------------------------------
2. Mahali anapoishi kwa sasa---------------------------------------------
3. Anwani ya mzazi/mlezi huyo ni --------------------------------------------
4 .Namba yake ya simu ni ------------------------------------------------------
5 .Kabila lake---------------------------------------------------------------------
6. Dhehebu/Dini-------------------------------------------------------------------
7.Jina la mwenyekiti wa kitongoji..........................................sahihi na Muhuri................
Mimi [ mzazi/mlezi atakayeandikishwa shuleni ]......................................ambaye ni mzazi/mlezi wa ............................[Jina la mwanafunzi] wa kidato.........mwaka.............
Nakiri kuwa nitakubaliana na kufuata sheria, kanuni na maelekezo mengine ya shule kadri yatakavyotolewa na uongozi wa shule.

**NITALIPA MICHANGO YOTE YA SHULE BILA USUMBUFU WOWOTE KWA SHULE WALA KWA MWANAFUNZI ILI KUMUWEZESHA MWANAFUNZI ASOME VIZURI.**
**NITAFUATILIA MAENDELEO YA MWANAFUNZI KILA MWEZI NA KUSHIRIKI VIKAO VYA KITAALUMA ILI KUHAKIKISHA MTOTO ANAKAMILISHA MALENGO YAKE**

| | |
|---|---|
| ................................................ | .............................. |
| mzazi/mlezi | Tarehe |

## AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE, KUTOSHIRIKI MIGOMO ,FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi [ mwanafunzi] ----------------------------------wa kidato-------- mwaka-------------naahadi kufuata sheria na taratibu zote za shule kadri zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule muda wote niwapo shuleni na kwamba sitashiriki migomo, fujo wala makosa yoyote ya jinai. Pia naahidi kuwa nitakuwa mwaminifu kwa uongozi wa shule na jumuiya nzima ya Nyampulukano Sekondari.

| | |
|---|---|
| -------------------------------- | --------------- |
| Saini ya mwanafunzi | Tarehe |

| | | |
|---|---|---|
| ............................ | ............................. | .......... |
| Jina la mzazi/mlezi | saini ya mzazi/mlezi | tarehe |

**SHULE YA SEKONDARI NYAMPULUKANO**

**FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

**1.** Jina kamili (Kama ilivyo kwenye *SEL - FORM*) ...........................................................................

**2.** Anwani ya nyumbani S.L.P ……………………………... WILAYA ...............................................

**3.** Tarehe ya kuzaliwa ………………..………………………………………………………………..…………

**4.** Mahali ulipozaliwa, Kijiji ……………………..……….. Kata ……..……………………………… Tarafa ………….….

**5.** Mahali unapoishi kwa sasa ………………………….…………………………. WILAYA ……….…………………………

**6.** Shule ya sekondari ulikotoka…………………………..……Anwani……………………………………….…….

**7.** Dini/Dhehebu ………………………………….…………….. Kabila ……………………………………………………

**8.** Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala yahusuyo shule:

**(i)** Jina la Baba ……………………………………………. Namba ya simu …………..………………….
Hai /Si hai …………………… (kama hai) kazi yake ……..………………… Anwani ……………..

**(ii)** Jina la mama ………………………………………….. Namba ya simu ………..……………….
Hai /Si hai…………………… (kama hai) kazi yake …….………….……. Anwani ………….………

**(iii)** Jina la Mlezi ………………………………... Uhusiano …………………… Namba ya simu …………......
kazi yake ……………..…………. Anwani S.L.P……………... WILAYA …………………………………

**NB: BANDIKA PICHA ZA WANAOHUSIKA HAPO JUU KWENYE VIBOMA**

| PASIPOTI BABA | PASIPOTI MAMA | PASIPOTI MLEZI |
|---|---|---|
| | | |

Mimi (Mwanafunzi) …………………………………………………………………………… nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

**………………………………………………..** **……………………**

**Saini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi) ………………………………………………………………………………. ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………………………………………………………………….. nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Nyampulukano ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha, naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

**………………………………………………..** **……………………**

**Saini ya Mzazi/Mlezi** **Tarehe**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**SENGEREMA DISTRICT COUNCIL**

**NYAMPULUKANO SECONDARY SCHOOL**

**MEDICALEXAMINATIONFORM**

**(TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER IN A DISTRICT HOSPITAL)**

**Student's full name……………………………………………………………….……..........**

**Age………………………… years ………………..  sex………………………………**

**Stool examination…………………………………………………………………….............**

**Urinalysis……………………………………………………………………..……….............**

**Blood count (red &white) ………………………………………………………….……........**

**Syphilis test……………………………………………………………….…………..........**

**Spleen………………………………………………………………………..……………...........**

**Mental condition…………………………………………………………….…………..........**

**Sight…………………………………………………………………………..……………...........**

**Chest (T.B) …………………………………………………………………………….............**

**Pregnancy ..……………………………………………………………………………............**

**ADDITIONAL INFORMATION (e.g. physical defects, impairments or chronic disease requiring special treatment/attention)**

**.............................................................................................................................................**
**.............................................................................................................................................**
**.............................................................................................................................................**
**.............................................................................................................................................**
**..........................................................................................................................................**

**I certify that I have examined the above student and recommend that he/she is fit/unfit to pursue his/her secondary education studies**

**Signature…………………………………………….**

**Designation………………………………………….**

**Official stamp……………………………………….**

**Date………………………………………………….**

**ORODHA YA VITABU**

**PHYSICS A - LEVEL**

1. S. CHAND'S PRINCIPLE OF PHYSICS FOR CLASS XI AND XII
2. ROGER MUNCHASTER
3. NELKON AND PARK. PRINCIPLE OF PHYSICS
4. UNIVERSITY PHYSICS (UP)
5. TOM DUNCAN

**BIOLOGY A – LEVEL**

1. COMPLETE ADVANCED BIOLOGY FORM 5 AND 6(Respicius Rwehumbiza)
2. ADVANCED LEVEL BIOLOGY TEXT FOR FORM 5 AND 6 (ERNEST KIRA)
3. BIOLOGY FOR SECONDARY SCHOOLS FORM FIVE (TIE)
4. NEW UNDERSTANDING BIOLOGY ( GLEEN AND SUSAN TOOLE)
5. BIOLOGICAL SCIENCE 3RD EDITION ( D.J TAYLOR; N.P.O GLEEN)

**CHEMISTRY A – LEVEL**

1. PRINCIPLES OF CHEMISTRY – BY CHAND CLASS XI, AND XII

**KISWAHILI**

1. FASIHI KWA UJUMLA
2. MAYOKA, J(1986) MGOGORO WA USHAIRI NA DIWANI YA MLOKA, DSM;TPH.
3. MDEE SEKONDARI; J.S (1988) SARUFI YA KISWAHILI SEKONDARI VYUO: DSM EDUCATION SERVICE CENTRE
4. VITABU TEULE

| A. RIWAYA | B;TAMTHILIYA | C; USHAIRI |
|---|---|---|
| (i) VUTA N'KUVUTE | (i) MORANI | (i) CHUNGUTAMU |
| (ii) MFADHILI | (ii) KIVULI KINAISHI | (ii) KIMBUNGA |
| (iii)USIKU UTAKAPOKWISHA | (iii) KWENYE UKINGO WA THIM | (iii) FUNGATE YA UHURU |
| (iv)KUFIKIRIKA | (iv) NGUZO MAMA | (iv) MAPENZI BORA |

**ENGLISH LANGUAGE**

1. KADEGHE,M (2010). THE REAL ENGLISH TEXT BOOK FOR ADVANCED LEVEL
2. (ASHELI, N (20100 2ND EDITION. ADVANCED LEVEL ENGLISH: A PRACTICAL APPROACH
3. **PLAYS:**
   A. BETRAYAL IN THE CITY, (FRANCIS IMBUGA)
   B. I WILL MARRY IF I WANT ( NGUGI WA THIONG'O
   C. THE BRIDE ( AUSTINE BUKENYA)
   D. LWANDA MAGERE ( OKOIT OMTATAH)
   E. AN ENEMY OF THE PEOPLE (HENRIK IBSEN)
   F. BLACK MAMBA ( JOHN RUGANDA)

4. **NOVELS AND SHORT STORIES**
    A. ENCOUNTERS FROM AFRICA(MACMILLAN PUBLISHERS)
    B. THE BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN ( AYI KWEI ARMAH)
    C. A MAN OF THE PEOPLE ( CHINUA ACHEBE)
    D. DEVINE PROVINCE (SEVERINE NDUNGURU)
    E. THE RAPE OF THE PEAR( MAGALA NYAGO)
    F. VANISHING SHADOWS ( NA MIGE KAYANDO)
    G. HIS EXCELLENCE THE HEAD OF STATE ( DANNY SAFO)
    H. A SEASON OF WAITING ( DAVID OMOWALE)
5. **POEM**
    A. SELECTED POEMS ( INSTITUTE OF EDUCATION)
    B. THE WONDERFUL SURGEON AND OTHER POEM ( CHARLES MLOKA)

**GEOGRAPHY**

A. MSABILA, D.T (2003). A COMPREHENSIVE APPROACH TO PHYSICAL GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOL
B. MSABILA, D.T (2008) . AN INTEGRATED REGIONAL STUDY ON HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY.
C. NJIKU, J.W & SALASU, J.F.K (2008) THE ESSENTIALS OF PRACTICALS GEOGRAPHY ADVANCED LEVEL FORM 5 & 6.
D. TRURAN, H.C . A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAP AND DIAGRAMS.
E. KAMIL, Z. PRACTICAL GEOGRAPHY ALIVES

**HISTORY**

A. KATO, A.K (2010) MASTERING ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER 1
B. KATO, A.K (2011) MASTERING ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER 2
C. CHIKU, M.D.J (2010) ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER TWO ALIVE AFRICA AND CRISIS OF CAPITALISM.
D. MWIJAGE, J.F.K (2004). MAJOR EVENTS IN AFRICA HISTORY.
E. RODNEY WALTER (1972. HOW EUROPE UNDERDEVELOP AFRICA.
F. NYERINDA, H.D. TOPICS IN AFRICA HISTORY FOR ADVANCED LEVEL CERTIFICATE, NOTES, HISTORY PAPER 1.

**GENERAL STUDIES.**

A. KADEGHE, M (2005). MODERN COMMUNICATION SKILLS ( THEORY AND PRACTICALS)
B. NYAMBARI C.M et al. CONTEMPORARY APPROACH FOR ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES

**ADVANCED MATHEMATICS**

A. PURE MATHEMATICS 1 ( L. BOSTOCK, S CHANDLER
B. S.CHAND'S MATHEMATICS FOR CLASS XI ( H.K DASS & DR. RAMA VERMA)

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**